

## **TUME YA UTUMISHI WA UMMA KUONGEZA VIWANGO VYA UTOAJI WA HUDUMA KWA WATANZANIA**

*Imetolewa na Ofisi ya Rais Tume ya Utumishi wa Umma.*

Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma inatarajia kuongeza na kuboresha zaidi viwango vya utoaji wa huduma kwa watanzania kutokana na mafunzo ya upimaji wa wazi wa utendaji wa kazi( OPRAS) ambayo yataongeza uwazi na uwajibikaji miongoni mwa watumishi na wapokeaji wa huduma zinazotolewa na Serikali

Katika mafunzo hayo(ambayo yanaendelea hivi sasa) watumishi wanafundishwa jinsi ya kutengeneza malengo mahususi kutokana na mpango mkakati wa taasisi, jinsi ya kujaza malengo mahususi kwenye fomu ya OPRAS na mahusiano yaliyopo baina ya malengo ya mtumishi binafsi na malengo ya taasisi. Aidha watumishi wanafundishwa Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma kuhusu OPRAS na changamoto zilizopo katika utumiaji wa mfumo wa OPRAS na namna ya kukubiliana na changamoto hizo.

Mafunzo ya OPRAS yana madhumuni ya kuboresha Utendaji kazi na uwajibikaji wa mtumishi wa umma, kuisitiza umuhimu wa ushirikishwaji, umiliki na uwazi katika kupanga malengo, utekelezaji wa malengo, mchakato mzima wa kufanya mapitio ya utendaji na kupima utendaji wa kazi wa mtumishi kwa kipindi cha mwaka mmoja.

Mafunzo ya OPRAS yataleta hamasa ya utekelezaji wa malengo kwa ufanisi zaidi, watumishi watakuwa na utendaji endelevu kwani utendaji wao wa kazi utatambuliwa na Menejimenti na yatawasaidia watumishi kufahamu upungufu wao kiujuzi na kujua hatua za kuchukua. Aidha mafunzo ya OPRAS yataisaidia Tume ya Utumishi wa Umma kupata mrejesho wa ufasaha ama udhaifu wa mifumo, michakato ama taratibu zilizopo katika ofisi yake, kupata fursa ya kutoa tuzo, adhabu kwa watumishi bila upendeleo. Aidha mafunzo hayo yataleta uwazi na uwajibikaji na kuipa Tume nafasi ya kujikita zaidi katika utekelezaji wa malengo yake.

Watumishi 82 wanashiriki katika mafunzo ya OPRAS. Makundi ya watumishi hao ni wasaidizi wa ofisi, walinzi na makatibu mahususi, maafisa mbali mbali, wahasibu wasaidizi, maafisa ugavi, wanasheria na madereva.

Mafunzo haya ambayo yanaendeshwa na Tume ya Utumishi wa Umma kupitia Mpango wa Maboresho ya Utumishi wa Umma awamu ya II kwa mwaka 2009/10 yanatolewa na Chuo cha Utumishi wa Umma cha Magogoni kilichopo Jijini Dar Es Salaam. Mafunzo haya ambayo yanatarajiwa kukamilika wiki ijayo yamefanyika kwa awamu nne ambapo awamu ya kwanza ilianza 23/11/2009 na kukamilika tarehe 27/11/2009.

Chimbuko la mafunzo ya watumishi katika utumishi wa umma ni Sera ya Menejimenti katika utumishi wa umma ya mwaka 1999 ambayo inaelekeza na kuanisha aina ya mafunzo na malengo ya mafunzo hayo. Lengo kubwa la mafunzo hayo ni kuhakikisha kuwa utumishi wa umma unaboreshwa ili kujenga mazingira mazuri ya ukuaji wa uchumi wa nchi ya Tanzania. Tume ya Utumishi wa Umma inazingatia maelekezo ya sera hii kutokana na mafunzo yanayoendeshwa kwa wakati huu. Aidha inaendesha mafunzo mengine ya muda mrefu na mfupi

**Iwapo una maoni au maswali tafadhali tuandikie**

**Katibu**

**Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma**

**S.LP 9143**

**Dar Es Salaam**